

## MBONA NIZINGATIE KUMTUNZA MWANANGU DHIDI YA MARADHI YA HEPATITIS C?

Maradhi ya Hepatitis C yanaweza kuadhiri afya ya mwanao kwa kipindi chote cha maisha yake. Asilimia 80 ya watoto walioambukizwa hepatitis C huugua kwa muda mrefu. Yasipotibiwa, yanaweza kusababisha madhara mabaya kwa maini. Watoto wengi walioambukizwa hepatitis C huonyesha ishara chache za maambukizi. Njia ya kipekee ya kujua kama mwanao anaugua maradhi ya hepatitis C ni kwa kupima damu.

## NASITAHILI KUFANYA NINI NIKIWA NA HEPATITIS C?

Baada ya kujifungua, tafuta matibabu ya hepatitis C.

Matibabu ya hepatitis C yatasaidia kuwalinda watoto utakaowapata baadaye dhidi ya hepatitis C, na pia kuilinda afya ya maini yako.

Jizuie kunywa pombe na utathmini matibabu yote na daktari, haswa kama unapokea matibabu ya ukimwi ama hepatitis B.



## WALINDE WAPENDWA WAKO

Watu wengine wanaweza kuambukizwa kupitia kwa damu ama kwa njia ya ngono bila kinga.

Usishiriki vitu vinavyoweza kuwa na damu kama vile sundano, wembe, miswaki, na kadhalika.

Unaposhiriki ngono, hakikisha unatumia kondomu.

Hakuna chanjo ya kumlinda mtoto ama mama dhidi ya hepatitis C.

Kwa habari zaidi, zungumza na mhadumu wa afya, piga Simu kwa idara ya afya, ama utazame Tovuti zifuatazo:

### Vituo vya Udhhibiti na Kuzuia Magonjwa:

[www.cdc.gov/hepatitis/hcv/cfaq.htm#overview](http://www.cdc.gov/hepatitis/hcv/cfaq.htm#overview)

[www.cdc.gov/hepatitis/hcv/hcvfaq.htm#g2](http://www.cdc.gov/hepatitis/hcv/hcvfaq.htm#g2)

### Fanya tathmini ya hatari ya hepatitis:

[www.cdc.gov/hepatitis/riskassessment/](http://www.cdc.gov/hepatitis/riskassessment/)

*Habari imetolewa na Idara ya Afya ya Umma ya Indiana*



Idara ya Mamlaka ya Afya ya Tennessee Authorization 3432 Hii stakabadhi ya Umma ilichapishwa kwa gharama ya dola 0.20 kwa kila nakala nakala 2500. 02-2020



# HEPATITIS C NA WANAWAKE WAJA WAZITO

Jee, umehatarishwa na hepatitis C?  
Jeep, wewe ni mja mzito ama unapanga



## HEPATITIS C NI NINI?

**Hepatitis C ni ugonjwa hatari wa maini** unaosababishwa na virus vya hepatitis C. Ugonjwa huu waweza kuendwlea kwa miaka, Hata miongo, bila dalili zozote hulu ukiendelea na adhari zake, zikiwemo cirrhosis (kuharibika kwa maini), kuzimia kwa maini, na saratani ya maini. Hatari ya kuambukizwa na hepatitis C inahusisha kudungwa sindano, kutumika sindano moja kudungwa, kupokea damu kabla ya 1992, kupokea hemodialysis ya muda mrefu, ama ushirika wa ngono na mtu aliye na hepatitis C.

## PERINATAL HEPATITIS C NI NINI?

Kama wewe ni mja mzito na umeambukizwa hepatitis C, mtoto wako pia anaweza kuambukizwa. Hii inajulikana kama perinatal hepatitis C. Perinatal hepatitis C ndiyo njia Kuu zaidi ya maambukizi kwa watoto. Kama asilimia sita ya watoto wanaozaliwa na mama walio na hepatitis C pia huambukizwa hepatitis C. Mama akiwa na ukimwi ama hepatitis B, uwezekano wa mtoto pia kuambukizwa hepatitis C huongezeka.

## MWELEZE DAKTARI WAKO

Hakikisha daktari wako anafahamu kuwa unaugua hepatitis C kama umedhibitishwa kuwa nayo. Hepatitis C ina tiba, lakini kwa sasa matibabu bado hayajathibitishwa kutumika na mama wenye mimba. Kuna njia za kuulinda afya yako pamoja na ile ya watu uwapendao. Kwa watoto walio hatarini kuambukizwa, kujua halo yao ni njia bora zaidi ya kupokea matibabu. Kwa hivyo, hakikisha pia wanapimwa hepatitis C.

## NI WAKATI UPI MWAFKA KWA MTOTO KUPIMWA HEPATITIS C?

**Baada ya umri wa miezi miwili**

**Pima hepatitis C RNA, ambayo hudhibitisha kama mwanao ana ushahidi wa maambukizi ya hivi punde.**

**Baada ya umri wa miezi kumina nane**

**Pima chembe chembe za hepatitis C, na kama ameambukizwa, pia pima hepatitis C RNA kuthibitisha.**

Chembe chembe za hepatitis C kwa umri huu huenda zikawa ni zile zimetoka kwa mama hadi kwa mtoto.

## JINSI GANI NAWENZA NIKAPIMWA HEPATITIS C?

**Zungumzana mhudumu wako wa afya, ama Idara ya Afya Karibu nawe**

**Pima chembe chembe za hepatitis C, na ikithibitika, pia pima hepatitis C RNA ili kuthibitisha maambukizi ya hivi punde.**

## FAHAMU KWA MAMA WENYE HEPATITIS C

**Swali. Jee, ni salama kumnyonyesha mwanangu?**

**Jibu.** Ndiyo! Hepatitis C haiambukizwi kupitia kwa matiti; Hata hivyo, zungumza na daktari wako kama unatokwa na damu kwenye matiti.

**Swali. Jee, nitumie njia ganikujifungua?**

**Jibu.** Waweza kujifungua kea njia ya kawaida ama kupasuliwa. Upasuaji na njia nyingine za kujifungua hazijadhibitika kuzuia maambukizi ya mama kwa mtoto ya hepatitis C.

**Swali. Jee, nikimkumbatia na Kumhusu mwanangu, ataambukizwa hepatitis C?**

**Jibu.** La, hepatitis C ihauambuzwi kupitia kwa mate, kukohoa, ama kuchefua. Unaambukizwa kwa damu ama ngono bila kinga na mtu aliyeambukizwa. Unaweza ukamkumbatia na Kumhusu mwanao bila kuhofia kumwambukiza maradhi ya hepatitis C.

